# Mfano wa kutokuhudhuria masomo Elimu ya Msingi Mji wa Jyväskylä

Anayeandaa masomo anatakiwa kuzuia kulikopangwa kabla kutokuhudhuria shuleni kwa mwanafunzi wa elimu ya msingi na pia kufuatilia na kuingilia kati kwa mpango. Anayeandaa masomo anatakiwa kutoa taarifa kutokuhudhuria bila ruhusa kwa mlezi wa mwanafunzi au mwakilishi mwingine halali. (Sheria ya Elimu ya Msingi 26 §)

Watoto wanaoishi kwa kudumu Finland wana wajibu wa masomo. Kwa mujibu wa sheria mzazi anawajibika kuhakikisha kuwa wajibu wa masomo unatekelezwa. (Sheria ya Wajibu wa Masomo 2 § na 9 §)

Kwenye kuhesabu kutokuhudhuria kwa mwanafunzi tunatilia maanani mara zote za kutokuhudhuria kwa mwaka mzima wa masomo, pia zilizopewa ruhusa. Kutokuhudhuria kunafuatiliwa kwa utaratibu maalum; kwenye kikundi cha matunzo ya wanafunzi mara nne kwa mwaka wa masomo.

## 1. Kuzuia kutokuhudhuria shuleni kulikopangwa kabla na kusaidia mahudhurio

### Shughuli zinazosaidia ustawi wa mwanafunzi, ushiriki na jumuiya

- Kuimarisha ujuzi wa hisia, usalama na mahusiano kati ya mwanafunzi na wafanyakazi.
- Wafanyakazi wanakutana na wanafunzi na kusaidia wanafunzi kujishikamanisha na shule kwa kuimarisha mipango ya ufundishaji na kusaidia vikundi maalum vinavyosaidia mazingira ya kujifunza.
- Wafanyakazi wanasaidia mahusiano kwenye vikundi na mahusiano ya rika, kutengeneza vikundi na kuzuia upweke katika safari nzima ya masomo.
- Jamii nzima inashiriki kutengeneza mazingira salama ya kujifunza na inaingilia kati kwenye kila ukatili, uonevu, uchokozi na ubaguzi.
- Wafanyakazi wanajenga mahusiano ya ushirikiano kati ya nyumbani na shuleni.
- Kutokuhudhuria kunafuatiliwa kwa mpango maalum kwa viwango binafsi na vya vikundi kama sehemu ya shughuli za huduma za masomo na mpango wa huduma za masomo.

## 2. Ingilia kati mara moja na fafanua pamoja na mwanafunzi na mlezi

- Mabadiliko yanayoleta wasiwasi kwenye tabia ya mwanafunzi
- Kutokutaka kuja shuleni
- Kuchelewa kila mara
- Kuondoka katikati ya kipindi au katikati ya siku ya shule
- Mwanafunzi yuko shuleni, lakini hayuko kwenye kipindi
- Kutokuhudhuria bila ruhusa
- Kutokuhudhuria bila maelezo au maelezo ya kutokuhudhuria yasiyotosheleza
- Kutokuhudhuria kila mara kwenye somo hilo hilo au kila siku fulani ya wiki

- Kutokuhudhuria kila mara na kwa muda mrefu

3. Kuingilia kati mapema 5 %

- Mwalimu anafafanua kutokuhudhuria kwa kuzungumza na mwanafunzi na mlezi.
- Mwalimu anafuatilia maendeleo ya kujifunza, anatambua matatizo ya kujifunza na anakadiria uhitaji wa msaada.
- Mwalimu anawasiliana kwa kizingiti cha chini na mwalimu maalum na wataalamu wa huduma za masomo, ikiwa kuna wasiwasi kwenye ustawi wa mwanafunzi, kujifunza au kuhudhuria shule.
- Ikihitajika mwalimu anakubaliana na mwanafunzi na mlezi wake kuhusu hatua za misaada na wakati ujao wa kuangalia tena.
- Kutokuhudhuria bila ruhusa na kusikokuwa na maelezo kunaingiliwa kati mara moja.

4. Hatua zenye malengo 10–15 %

- Mwalimu anawasiliana na walezi na anaomba ikihitajika ruhusa ya kukusanya kikundi cha wataalamu mbalimbali na msaada binafsi wa huduma za masomo.
- Ikihitajika mwalimu anawasiliana na walimu maalum na wataalamu wa huduma za masomo.
- Mwalimu anakusanya kikundi cha wataalamu mbalimbali, ikiwa inaonekana kinahitajika kwa ajili ya ustawi wa mwanafunzi, kujifunza au mahudhurio yake.
- Kwenye mkutano wanachunguza sababu zilizo nyuma ya kukosa kuhudhuria na kuimarisha maandalizi ya ufundishaji na aina za misaada ya vikundi maalum zinazosaidia mazingira ya kujifunza. Vilevile watakubaliana kuhusu malengo, hatua za misaada za shuleni na nyumbani, mtu anayewajibika na wakati unaofuata wa kuangalia upya.
- Ikiwa kikundi cha wataalamu mbalimbali hakikukusanywa, mwalimu anakubaliana pamoja na mwanafunzi na mlezi wake kuhusu hatua za misaada, ufuatiliaji na hatua zinazolenga jamii nzima.

5. Hatua madhubuti 20 %

- Kukadiria uhitaji wa msaada binafsi kwa mwanafunzi kama sehemu ya mpango wa utekelezaji wa msaada binafsi.
- Mwalimu anakusanya kikundi cha wataalamu mbalimbali. Ikihitajika kushauriana na watendaji kutoka nje ya shule.
- Walimu na wataalamu wa huduma za masomo wanakubaliana kutengeneza ramani ya sababu za kutokuhudhuria pamoja na mwanafunzi na walezi wake.
- Ikiwa mpango binafsi wa mwanafunzi utasababisha kutolewa uamuzi unaohusu msaada, msaada utaandaliwa kulingana na mpango.
- Mtu anayewajibika anahakikisha utekelezaji wa hatua za misaada zilizokubaliwa kwenye mpango na anadumisha mahusiano na mwanafunzi.
- Ikihitajika mwalimu anafanya 1) kwa mujibu wa Sheria ya Ustawi wa Jamii mawasiliano ya kukadiria uhitaji wa msaada au 2) taarifa ya ulinzi wa watoto.

6. Ikiwa kutokuhudhuria kutaendelea

- Kuimarisha na kueleza bayana ushirikiano kati ya wadau mbalimbali.
- Ikihitajika uhitaji wa msaada binafsi kwa mwanafunzi unafafanuliwa na mpango wa utekelezaji wa msaada binafsi kwa mwanafunzi unatengenezwa upya.
- Mtu anayewajibika atamsaidia mwanafunzi kurudia shuleni kwa mpangilio.

10 % ya kutokuhudhuria imechunguzwa kuwa ni kitu cha hatari kwa ustawi na kujifunza.

Asilimia ya kutokuhudhuria na saa za mwaka wa masomo Jyväskylä

| **DARASA** | **5 % KUTOKUHUDHURIA** | **10 % KUTOKUHUDHURIA** | **15 % KUTOKUHUDHURIA** | **20 % KUTOKUHUDHURIA** |
|---|---|---|---|---|
| Darasa la 1.–2. | saa 40 | saa 80 | saa 120 | saa 160 |
| Darasa la 3. | saa 44 | saa 87 | saa 131 | saa 175 |
| Darasa la 4. | saa 46 | saa 91 | saa 137 | saa 182 |
| Darasa la 5.–6. | saa 48 | saa 95 | saa 143 | saa 190 |
| Darasa la 7.–9. | saa 57 | saa 114 | saa 171 | saa 228 |

Taarifa ya kutokuhudhuria ya Wilma inatumwa moja kwa moja kwa mujibu wa viwango vya masaa yaliyoko kwenye jedwali hili.